**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**


**IRINGA REGIONAL**

Tel: 026-2702264

Fax No.: 026-2702264

HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA

S.L.P 260

**IRINGA**


# MKATABA WA UFUNDI WA UKARABATI WA JENGO LA ICU:

# KAZI YA UBOMOAJI WA UKUTA KATIKA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA IRINGA

**MWAJIRI**

MGANGA MFAWIDHI

**IRINGA**

**FUNDI**

MKUU WA MAGEREZA MKOA

**IRINGA**

**DESEMBA- 2021**

# FOMU YA MKATABA

## MKATABA WA UFUNDI WA UKARABATI WA JENGO LA ICU

## KAZI YA KAZI YA UBOMOAJI WA KUTA KATIKA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA IRINGA

Makubaliano haya ya mkataba wa ufundi wa ukarabati wa jengo la icu, kazi ya ubomoaji wa kuta katika hospitali ya rufaa ya mkoa iringa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Iringa yamefanyika leo tarehe ....21.....ya mwezi wa.12 mwaka ....2021

**KATI YA**

**Mganga Mfawidhi , S.L.P. 260 Iringa**, ambaye kwa madhumuni ya mkataba huu atajulikana kama (Mwajiri) kwa upande mmoja,

**MKUU WA MAGEREZA-IRINGA**, ambaye kwa madhumuni ya mkataba huu anajulikana kama ***"Fundi "*** kwa upande mwingine.

**Kwa kuwa,** Mwajiri anahitaji ukarabati wa jengo la ICU) kwa kutumia njia ya usimamizi na rasilimali za ndani (***Force Account***) ;

**Kwa kuwa,**Katika kutekeleza azma yake, Mwajiri amezingatia taratibu, kanuni na Sheria ya Manunuzi Namba 7 ya mwaka 2011;

**Na kwa kuwa,** mwajiri kupitia ridhaa iliyotolewa na Bodi ya Zabuni ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa kupitia *kikao cha dharura cha tarehe 16/12/2021* iliridhia kazi ya ubomoaji wa kuta apewe Mkuu wa Magereza wa Mkoa sawa na mchanganuo umbeambatanishwa kwa gharama ya Shilingi za Kitanzania milioni mbili laki tisa tu, (TShs 2,900,000/=) ambayo ni bei ya Mkataba kwa muda wa Siku...14.....kuanzia tarehe ya kusainiwa kwa mkataba

**HIVYO BASI, PANDE ZOTE MBILI ZIMEKUBALIANA KUFUNGWA NA MASHARTI YA MKATABA KAMA IFUATAVYO:-**

## MAANA YA MANENO NA MAELEZO

Katika makubaliano haya, maneno na maelezo yatakuwa na maana sawa kama yalivyopewa katika masharti ya mkataba unaojieleza.

## MUDA WA MKATABA

Kwamba pande mbili katika mkataba huu zimekubaliana kuwa Muda wa kuanza hadi kumaliza kazi ni Majuma matatu, na kwamba muda huu utaanza kuhesabika siku na tarehe ya kukabidhiwa site .

## MALIPO YA FIDIA/HASARA

i. **Kwamba Fundi** atawajibika kumlipa Mwajiri hasara za vifaa vyote pamoja na gharama nyinginezo zitakazotokana na kazi zisizoridhisha kwa mujibu wa mkataba huu.

ii. Kwamba, Fundi atamlipa mwajiri asilimia thelathini (30%) ya kazi ambayo hajamaliza kwa wakati itakayosababisha mwajiri kuingia gharama nyingine ya ziada.

iii. Ofisi ya Mganga Mfawidhi inaridhia **Mkuu wa Magereza Mkoa wa IRINGA** apewe kazi ya ukarabati wa jengo la icu , kazi ya ubomoaji wa kuta kwa gharama ya Shilingi za Kitanzania Milioni mbili laki tisa tu, (TShs 2,900,000/=) ambayo ni bei ya Mkataba

iv. **HIVYO BASI, PANDE ZOTE MBILI ZIMEKUBALIANA KUFUNGWA KWA MKATABA -**

## TARATIBU ZA MALIPO YA KAZI NA MAPOKEZI YA VIFAA VYA UJENZI.

Imekubalika na pande mbili katika mkataba huu Kwamba,vifaa(Building materials)vitakavyotumika katika kazi vitatolewa na Mwajiri, na kwamba Fundi atalipwa gharama za ufundi (Labour Charge). Kama ilivyoainishwa katika Utaratibu wa ufanyaji kazi (Schedule of Activity na ramani).

Ni wajibu wa fundi kutafuta vifaa vya kufanyia kazi (Mfano mwiko, pima maji, kamba, tape measre n.k). Mwajiri hatawajibika na upatikanaji wa vifaa hivyo.

Kwamba, pande mbili katika mkataba huu zimekubaliana kuwa katika kipindi chote cha mkataba huu Fundi atatakiwa kuwa na Akaunti katika Benki inayofikika kirahisi.

**MALIPO**

v. Fundi atalipwa kiasi cha kwa gharama ya Shilingi za Kitanzania milioni mbili laki tisa tu, (TShs 2,900,000/=) ambayo ni bei ya Mkataba **[Thamani ya Mkataba]**.Fedha hizi zitakuwa zinalipwa kila baada ya Fundi kutekeleza majukumu yake na baada ya ukaguzi wa ubora wa kazi na hatua iliyofikiwa

(i) Gharama za ufundi zilizoainishwa kwenye Mkataba huu ndizo zitakazohusika kwenye malipo.
(ii) Malipo yatafanyika kwa Shilingi za Kitanzania.
(iii) Malipo yatafanyika pale tu nyaraka zifuatazo zitakapokuwa zimekamilika na kuwasilishwa pamoja na maombi:-
  a) Barua ya Maombi ya kulipwa kutoka kwa Fundi iliyoainisha kazi alizofanya kulingana na mpango kazi uliowasilishwa kabla ya kusainiwa kwa mkataba huu.
  b) Taarifa ya kamati ya Ujenzi pamoja na Taarifa ya Mhandisi Msimamizi.

**WAJIBU WA FUNDI**

Katika mkataba huu Fundi atakuwa na wajibu wa kutekeleza yafuatayo;

(i) Atafanya kazi ya ukarabati wa jengo la icu, kazi ya ubomoaji wa kuta kama ilivyoainishwa kwenye 'Schedule of Activity' ambayo ni sehemu ya mkataba huu.
(ii) Kuwalipa vibarua wote anaofanya nao kazi.
(iii) Kukabidhi kazi yenye ubora iliyokidhi viwango na mahitaji ya mwajiri.
(iv) Kuwepo eneo la kazi muda wote kazi inapofanyika.
(v) Kutumia vifaa vya ujenzi alivyokabidhiwa kwa uangalifu na uaminifu.
(vi) Endapo kazi itakataliwa na kutokupokelewa kwasababu yakutokidhi viwango vilivyoainishwa, Fundi atarudia kazi hiyo kwa gharama (gharama za vifaa na ufundi) zake mwenyewe.

(vii) Atawajibika na usalama mahali pa kazi siku zote za kazi.
(viii) Kuhakikisha anamaliza kaziya ya ubomoaji ndani ya muda ulioainishwa kwenye mkataba huu.
(ix) Kuwasilisha barua ya Maombi ya Malipo baada ya kukamilisha kazi kwa kuzingatia mpango kazi uliokubalika
(x) Kutoa Ushirikiano kwa wasimamizi wa kazi

**WAJIBU WA MWAJIRI**

Katika mkataba huu mwajiri atakuwa na wajibu wa kutekeleza yafuatayo.

(i) Kuhifadhi na Kutoa vifaa kwa awamu pale vinapohitajika na Fundi kwa ajili ya kazi ya ubomoaji wa kuta.
(ii) Kukagua kazi ya ukarabati wa jengo mara kwa mara ili kuhakikisha ukarabati huo unakidhi vipimo, ubora na viwango kwa mujibu wa maelekezo yaliyotolewa kwa Fundi.
(iii) Kununua vifaa vinavyohitajika katika kazi ya ubomoaji wa kuta rangi, na Kumlipa Fundi kulingana na kazi iliyofanyika.
(iv) Kutoa ithibati kwa kazi iliyofanyika na hivyo kuridhia kiwango cha kazi iliyofanyika.
(v) Kuteua msimamizi wa kazi hiyo .

**UKAGUZI**

(i) Mwajiri ana haki ya kukagua kazi ya ubomoaji kuta kwenye ukarabati wa jengo la ICU ili kujiridhisha na ubora kama ilivyoainishwa kwenye mkataba.
(ii) Mwajiri ana haki ya kukataa ukarabati uliofanyika chini ya viwango vilivyowekwa.
(iii) Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi atamwakilisha mwajiri kwenye ukaguzi wa mara kwa mara wakati wa ukarabati.

**KUVUNJIKA/KUSITISHWA MKATABA**

(i) Upande wowote unaweza kuvunja au kusitisha mkataba muda wowote kwa kutoa notisi ya maandishi ya siku saba.

(ii) Endapo Fundi atashindwa kukamilisha kazi ya ubomoaji wa kuta kwa muda wa mkataba au kufanya chini ya kiwango tofauti na makubaliano, mwajiri atalazimika kuvunja au kusitisha mkataba na Fundi atalazimika kulipa fidia ya hasara zitakazojitokeza kutokana na kuvunjika kwa mkataba huu.

## MAJANGA YA KIASILI

(i) Kwamba, endapo itatokea kazi ya ukarabati wa jengo la icu, kazi ubomoaji wa kuta kama ilivyoainishwa imeathiriwa au itaathiriwa na visababishi vya asili kama vile mafuriko, tetemeko la asili, magonjwa ya mlipuko na ukame, Fundi atapaswa na kuwajibika kutoa taarifa mapema kwa Mwajiri ili kuona na kutathmini ni kiasi gani visababishi hivyo vimeathiri au vitaathiri ujenzi wa jengo la Magonjwa ya dharura hiyo.

(ii) Kwamba, kwa kuzingatia masharti yaliyopo kwenye kifungu (i) hapo juu, ni lazima Mwajiri aridhike na sababu zitakazotolewa na Fundi kuwa ni za msingi na zimeathiri au zitaathiri ujenzi wa jengo la Magonjwa ya dharura hiyo.

## SHERIA NA UTATUZI WA MIGOGORO

(i) Kwamba, mkataba huu utatekelezwa na pande zote kwa mujibu wa sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania za mikataba na sheria ya manunuzi ya Umma.

(ii) Kwamba, endapo mgogoro wowote utatokea kuhusiana na utekelezaji wa mkataba huu utasuluhushwa na wahusika wa pande zote mbili kwa amani na endapo upande wowote hautaridhika na mwafaka uliofikiwa, utaratibu wa utatuzi wa migogoro ya kimikataba utafuatwa

**MAKUBALIANO**

Kwa kuthibitisha mkataba huu, pande zote mbili zinaweka saini zao bila kushurutishwa na mtu kama inavyoonekana hapa chini, leo tarehe ....................

**UPANDE WA MWAJIRI UMESAINIWA NA:**

**Jina:** DR. IDDY OMARY

**Sahihi:** ...........................

**Cheo:** Ag MOI.

**Tarehe:** 20/12/2021

FOR: MEDICAL OFFICER INCHARGE
P.O.BOX 260
IRINGA

**Jina** Nebiotth Lukosi

**Sahihi:** ...........................

**Cheo:** Mhasibu

**Tarehe:** 20/12/2021

**UPANDE WA FUNDI UMESAINIWA NA:**

**Jina:** MATHIAS K. MKAMA

**Sahihi:** ...........................

**Cheo:** RPO (ACP)

**Tarehe:** 21/12/2021

MKUU WA MAGEREZA
MKOA WA IRINGA

**Jina** OSDO L. MALLONDO

**Sahihi:** ........................... SP.

**Cheo:** AFISA MNADHIMU

**Tarehe:** 21/12/2021